

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21 – 30 SEPTEMBER, 2018 NA MATARAJIO YA MVUA KWA SIKU KUMI ZA MWANZO ZA MWEZI OKTOBA (01– 10 OKTOBA, 2018)

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21–30 SEPTEMBER, 2018

Katika siku 10 za mwisho za mwezi Septemba 2018, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Ukanda wa mvua wa (ITCZ) uliendelea kubaki kaskazini zaidi hata hivyo sehemu yake ilikaribia maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria. Pepo kutoka kusini-mashariki zilivuma katika maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la wastani lilishuhudiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hali iliyopunguza uwezekano wa kutokea kwa vimbunga baharini. Eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilikuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilipelekea kupunguza kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21–30 SEPTEMBER, 2018

Mwenendo wa viashiria vya hali ya hewa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo katika ameneo ya ukanda wa ziwa Victoria. Pia pepo zivumazo kutoka kusini mashariki zilipelekea vipindi vichache vya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2018.

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2018)

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kubaki kaskazini Zaidi lakini sehemu yake inatarajiwa kuendelea kukaribia maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria. Pia pepo kutoka kusini-mashariki zinatarajiwa kuendelea kuvuma katika maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi na kusababisha uwepo wa hewa ya unyevunyevu. Uwezekano wa kutokea kwa vimbunga baharini kwa kipindi hiki ni mdogo. Eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kuongezeka kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kusababisha uwepo wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 OKTOBA, 2018)

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,): Mawingu kiasi kwa ujumla.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua katika maeneo machache hususani wiki ya pili

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mawingu kiasi kwa ujumla.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Mawingu kiasi.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Mawingu kiasi kwa ujumla.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Mawingu kiasi.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**